**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KUTOKA KWENYE SEKTA MBALI MBALI ILIYOWASILISHWA KWENYE KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI MKOA (RCC) TAREHE 28/9/2017.**

## SEKTA YA ELIMU

Mkoa wa Lindi wenye halmashauri 6 unazo taasisi mbalimbali za elimu zilizoanzishwa na serikali kwa lengo la kujenga taifa la watu thabiti, wenye misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi, umahiri na uwezo wa kujitegemea katika dunia ya maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia (Sera ya Elimu na Mafunzo 2014).

Taasisi zenye dhamana ya utoaji elimu zilizopo katika Mkoa wa Lindi ni shule za msingi 498, shule za sekondari 122, chuo cha ualimu 1, vyuo vya maendeleo ya jamii 2, chuo cha VETA 1, chuo kikuu huria 1, taasisi ya elimu ya watu wazima 1, vituo vya ufundi stadi 14 na shule zenye mkondo maalum 6 na vituo vya MEMKWA 49. Pamoja na taasisi zilizotajwa kuna shule shikizi (satellite schools) 44 ambapo kila halmashauri ina shule za namna hiyo ambazo baadaye zitakuwa shule kamili.

## TAARIFA ZA WANAFUNZI

Mkoa una jumla ya wanafunzi wa shule za msingi (darasa la I – VII) 202,762 wakiwemo wavulana 100,807 na wasichana 101,955. Kwa upande wa elimu ya sekondari wanafunzi waliopo ni 29,222 wakiwemo wavulana 14,864 na wasichana 14,358. Wanafunzi waliopangwa kujiunga kidato cha tano walikuwa 1,462 na walioripoti mpaka tarehe 18 Septemba, 2017 ni 1002. Hivyo, wanafunzi 460 hawakuripoti kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kubadilishiwa shule na wengine kujiunga na shule za binafsi.

Taarifa ya uandikishaji kwa mwaka 2017, kwa wanafunzi wa awali maoteo yalikuwa 29,920 (wav 14,828 na was 15,092), uandikishaji halisi ni 29,567 sawa na asilimia 99 (wav 14,524 na was 15,043). Wanafunzi wa darasa la kwanza maoteo 28,667 (wav 14,495 na was 14,172) uandikishaji halisi ni wanafunzi 36,246 sawa na asilimia 126.4 (wav 18,527 na was 17,719.

## TAARIFA ZA WALIMU

Ili ufundishaji na ujifunzaji uwe fanisi na wenye matokeo chanya kunahitajika pawepo na walimu wenye umahiri kwa ajili ya kutoa maarifa kwa wanafunzi waliopo. Mahitaji ya walimu kwa elimu ya msingi ni 5,104, walimu waliopo ni 3,721 na upungufu ni 1,383. Katika elimu ya sekondari upungufu wa walimu upo kwa walimu wa sayansi ambapo mahitaji halisi ni walimu 716, waliopo 243 na upungufu ni walimu 473 ambao ni sawa na 66.1%.

Katika jitihada za serikali za kuajiri walimu wapya, mkoa ulipangiwa walimu 103 wa sayansi awamu ya kwanza mwezi Aprili, 2017 na walioripoti ni walimu 96, walimu 7 hawakuripoti. Awamu ya pili mkoa ulipangiwa walimu 17 wa sayansi na hisabati na walioripoti ni walimu 8 na wasioripoti ni walimu 9. Mkoa hauna upungufu wa walimu wa masomo ya sanaa.

## MIUNDOMBINU YA SHULE ILIYOPO

Miundombinu ni eneo muhimu sana katika kufanikisha suala zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi. Katika elimu ya msingi mahitaji ya vyumba vya madarasa ni 4,908 na vilivyopo

ni 3,101 na upungufu ni 1,804. Kwa upande wa nyumba za walimu mahitaji ni nyumba 4,262 zilizopo 1,270 na upungufu 2,993.

Kwa upande wa elimu ya sekondari kuna upungufu wa miundombinu kama ifuatavyo: mahitaji ya vyumba vya madarasa 833, vilivyopo 800 na upungufu 33, nyumba za walimu mahitaji ni 1,628, zilizopo 390, upungufu 1,238, vyumba vya maabara mahitaji ni 345 vilivyopo 114 na upungufu 231. Aidha, katika matundu ya vyoo pia kumekuwa na upungufu mkubwa ukilinganisha na idadi ya wanafunzi waliopo kwa elimu ya msingi na sekondari.

**MIRADI INAYOYOTEKELEZWA KATIKA MKOA**

Mkoa umekuwa ukitekeleza miradi/programu mbalimbali ikiwemo EQUIP- Tanzania katika halmashauri zote 6. Mpaka mwezi Agosti, 2017 kiasi cha Tsh. 8,458,143,629 kilipokelewa katika halmashauri za mkoa huu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za program ya Equip-T. Programu ya LANES inatekelezwa katika halmashauri ya Wilaya ya Liwale (shule shikizi 10) na ikihusika na vituo vya MEMKWA kwa halmashauri 6. Pia miradi chini ya mpango wa EP4R inayohusika na fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mkoa umekuwa ukisimamia kwa karibu kuhakikisha dhima ya serikali inafikiwa.

**UENDESHAJI WA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2017**

Mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) mwaka 2017 umefanyika kuanzia tarehe 6 na 7 Septemba, 2017 nchini kote. Kwa mkoa wa Lindi mtihani huu umefanyika katika shule 480 zenye jumla ya wanafunzi 17,519 wakiwemo wavulana 8,117 na wasichana 9,402 katika halmashauri 6 za mkoa wa Lindi. Aidha, mtihani huo ulifanyika katika mazingira ya utulivu, amani na usalama katika halmashauri zote.

## TAARIFA ZA WATAHINIWA

### Waliosajiliwa na waliofanya Mtihani

Jumla ya Wanafunzi 26,804 waliandikishwa kuanza darasa la I mwaka 2011, wanafunzi 17,519 walisajiliwa kufanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2017. Aidha, wanafunzi 17,392 (99.3%) walifanya Mtihani na wanafunzi 127 (0.7%) hawakufanya Mtihani huo kutokana na sababu mbalimbalikama inavyooneshwa katika jedwali na 1 na 2.

### JEDWALI NA 1: MCHANGANUO WA WANAFUNZI WALIOFANYA MTIHANI

| **Halmashauri** | **WALIOANDIKISHWA 2011** | | | **WALIOSAJILIWA** | | | **WALIOFANYA MTIHANI** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **WV** | **WS** | **JML** | **WV** | **WS** | **JML** | **WV** | **WS** | **JML** | **%** |
| Kilwa | 3080 | 3050 | 6130 | 1931 | 2107 | 4038 | 1901 | 2078 | 3979 | 98.5 |
| Lindi | 2974 | 3303 | 6277 | 1629 | 2010 | 3639 | 1614 | 1993 | 3607 | 99.1 |
| Lindi Manispaa | 1006 | 1036 | 2042 | 729 | 815 | 1544 | 729 | 813 | 1542 | 99.9 |
| Liwale | 1452 | 1497 | 2949 | 1031 | 1169 | 2200 | 1026 | 1167 | 2195 | 99.6 |
| Nachingwea | 2617 | 2673 | 5290 | 1705 | 1894 | 3599 | 1696 | 1883 | 3579 | 99.4 |
| Ruangwa | 2085 | 2031 | 4116 | 1092 | 1407 | 2499 | 1086 | 1404 | 2490 | 99.6 |
| **JUMLA** | **13214** | **13590** | **26804** | **8117** | **9402** | **17519** | **8052** | **9338** | **17392** | **99.3** |

### JEDWALI NA 2: MCHANGANUO WA WANAFUNZI WASIOFANYA MTIHANI

| **Halmashauri** | **UTORO** | | | **VIFO** | | | **UGONJWA** | | | **SABABU NYINGINE** | | | **JUMLA** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WV | WS | JML | WV | WS | JML | WV | WS | JML | WV | WS | JML | WV | WS | JML |
| Kilwa | 27 | 19 | 46 | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 4 | 0 | 7 | 7 | 30 | 29 | 59 |
| Lindi | 15 | 10 | 25 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 6 | 6 | 15 | 17 | 32 |
| Lindi Manispaa | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Liwale | 4 | 2 | 6 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 2 | 7 |
| Nachingwea | 8 | 8 | 16 | 1 | 0 | 1 | 0 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 9 | 11 | 20 |
| Ruangwa | 3 | 3 | 6 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 3 | 9 |
| **JUMLA** | **57** | **43** | **100** | **6** | **1** | **7** | **2** | **7** | **9** | **0** | **13** | **13** | **65** | **62** | **127** |

Aidha, kwa mwaka 2017, Mkoa wa Lindi una jumla ya Wanafunzi 35 wakiwemo wavulana 17 na wasichana 18 ambao hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu waliofanya mtihani huu.

## MAANDALIZI YA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) MWAKA 2017

Mkoa umeendelea na maandalizi ya kufanyika kwa mtihani huo kwa kuendelea kusimamia ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya shule kwa kila mwalimu. Walimu wakuu, waratibu elimu kata, wakaguzi na maafisa elimu ngazi ya wilaya wamekuwa wakisisitizwa kusimamia na kuhakikisha kazi ya ufundishaji na ujifunzaji inafanyika kikamilifu. Pia mkoa umeendesha mtihani wa dhihaki kwa shule zote za sekondari za serikali na zisizo za serikali na kutoa matokeo. Katika mtihani huo watahiniwa 3,878 kati ya watahiniwa waliosajiliwa 4,010 walifanya matihani.

Matokeo ya mtihani huo yanaonesha ufaulu wa daraja I – III ni watahiniwa 636 (16.4%), daraja la IV ni watahiniwa 2187 (56.4%) na daraja la 0 wamepata watahiniwa 1050 (27.1%). Halmashauri pia zimekuwa na mitihani inayoendeshwa na kusimamiwa vyema ikiwa ni jitihada za kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya mtihani wa kidato cha nne utakaofanyika mwezi Novemba mwaka 2017 nchini kote. Jitihada zinazofanyika kwa kidato cha nne pia zimekuwa zikisisitizwa kufanyika kwa vidato vyote ngazi ya shule.

**MAANDALIZI YA WANAFUNZI KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2018**

Mkoa wa Lindi wenye jumla ya shule za sekondari 116 zilizo za serikali unatarajia kupokea wanafunzi 17,392 (99.3%) wa kidato cha kwanza mwaka 2018. Idadi hiyo ya wanafunzi ndio waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) mwaka 2017. Hivyo basi, vyumba vya madarasa vitakavyohitajika kwa ajili ya wanafunzi hao ni 435 ikilinganishwa na vyumba 246 vilivyohitajika mwaka 2017 kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wapatao 9,879 (65.16%) waliofaulu. Ili kuepukana na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa ni wajibu wa kila halmashauri kufanya maandalizi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa mapema kabla ya zoezi la uchaguzi wa wanafunzi hao halijafanyika.

Mwezi Januari, 2017 halmashauri ya Kilwa (shule ya sekondari Kilwa Kivinje, Ali Mchumo, Kiranjeranje na Mpunyule) na halmashauri ya Ruangwa (shule ya sekondari Ruangwa, Chinongwe, Mnacho, Namichinga na Hawa Mchopa) zilikuwa na miundombinu pungufu iliyopelekea wanafunzi waliofaulu kubaki bila kupangwa. Hivyo, ni jukumu la kila halmashauri kujiandaa kwa ajili ya mapokezi ya wanafunzi hao ili isije ikajitokeza wakati wa zoezi la uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2018 wanafaunzi wanabaki bila kupangwa katika shule husika kwa kukosa vyumba vya madarasa.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA ELIMU**

Mkoa wa Lindi katika utekelezaji wa kazi za Sekta ya elimu unakumbana na changamoto mbalimbali miongoni mwa changamoto hizi ni: -

i. Upungufu miundombinu na samani muhimu katika shule za msingi na Sekondari.
ii. Mwitikio mdogo wa wazazi/jamii kuwekeza katika sekta ya elimu kwa watoto wao kwa kuchangia na kugharamia elimu ya watoto wao.
iii. Usimamizi na ufuatiliaji hafifu wa wazazi/walezi katika mchakato wa kujifunza kwa watoto wao. Watoto wengi kuishi na kulelewa bila wazazi wao. Mfano: Manispaa ya Lindi kati ya wanafunzi 2,807 wa darasa la VII ni wanafunzi 562 tu (20.02%) ndiyo wanalelewa na wazazi wote wawili, aidha, kati ya wanafunzi wote 13,235 ni wanafunzi 5,824 sawa na 44.0% wanaokaa kwa wazazi wao wote wawili (utafiti: Feb. 2016)
iv. Ushiriki mdogo wa wazazi/walezi katika kudhibiti nidhamu za watoto wao na hivyo kusababisha wanafunzi kujiingiza kwenye makundi mbalimbali yasio na tija
v. Upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

## MIKAKATI YA KUKABILI CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA ELIMU NA KUINUA TAALUMA KATIKA MKOA

Baadhi ya mikakati ya kukabili changamoto za sekta ya elimu katika mkoa ni pamoja na;

i. Kuendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kujenga madarasa, vyoo, nyumba za walimu, maabara na kutengeneza madawati na samani kwa kushirikisha Serikali kuu, Halmashauri, wananchi na wahisani.

ii. Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji ngazi za shule, kata, wilaya na mkoa na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wote wanaokiuka maadili ya kazi.

iii. Kuendelea kurekebisha ikama ya walimu kwa kuzingatia mahitaji ya kila shule.

iv. Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuthamini na kushiriki kusimamia na kufuatilia mchakato wa ujifunzaji kwa watoto wao na kuchangia nguvu kazi na rasilimali zingine za kuimarisha shule katika maeneo yao.

v. Wilaya zote kuhakikisha wanafunzi wanaofaulu kuingia kidato cha I kila mwaka na wanaoandikishwa darasa la I wanafuatiliwa na wanasimamiwa kuhudhuria shule wakati wote wa masomo.

vi. Kuendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu ya kumudu stadi za KKK kwa wanafunzi wa darasa I & II na kuhakikisha watoto wote wanaoingia darasa la III kila mwaka wanamudu stadi za KKK.

## SEKTA YA AFYA

### TAARIFA YA HALI YA DAWA

Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu kwa kipindi cha 2016/2017 iliongezeka kwa 50% ikilinganishwa na ile ya mwaka 2015/2016. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2016 – Juni 2017 mkoa ulipokea Tsh. 538,398,818 kwa ajili ya ununuzi wa dawa kupitia bohari ya dawa.

Hospitali ya Mkoa ilipokea Tsh. 195,328,186 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na pia ilitumia Tsh. 127,171,700 toka fedha za uchangiaji kwa ununuzi wa dawa. Katika kipindi hiki upatikanaji wa dawa uliongezeka toka 67.2% hadi 74.9%. Aidha, katika halmashauri ununuzi wa madawa kwa kutumia fedha za uchangiaji ilikuwa kama ifuatavyo; Ruangwa Tsh. 12,027,000/=, Liwale Tsh. 32,000,000/=, Lindi manispaa Tsh. 27,495,100/= na halmashauri ya wilaya ya Lindi Tsh. 23,210,037.87/=.

### UKARABATI WA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA – SOKOINE

Tunaendelea na uboreshaji wa hospitali ya rufaa ya mkoa Sokoine kwa kufanya ukarabati wa wodi namba 6, wodi ya daraja la kwanza (grade I), na wodi ya wazazi kwa kutumia fedha kutoka katika mfuko wa LIDEF. Kwa wodi namba sita tumeikarabati yote kwa kugawa vyumba vidogo vidogo (''Partition"), kuweka malumalu (''tiles"), dari (''gypsum board), vyoo, kupaka rangi, na ukarabati wa mfumo wa maji safi na maji taka upo katika hatua za mwisho. Tumejenga kichomea taka cha kisasa (''High Tech Incinerator") na kimeshaanza kufanya kazi. Kazi hizi zimekamilika kinachosubiriwa ni majengo hayo kuanza kutoa huduma.

Hospitali ya mkoa ya rufaa imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya kuharibika mara kwa mara kwa mashine ya X-RAY kutokana na mashine hiyo kuwa ya muda mrefu hali inayosababisha ugumu na gharama ya upatikanaji wa vipuri kwa ajili ya matengenezo. Kwasasa mashine hii imekarabatiwa na inatoa huduma wakati taratibu za kupata mashine nyingine zinaendelea.

Pia hospitali ya mkoa ina jengo la ''ICU'' na vifaa vyote lakini kwa muda mrefu halitumiki kutokana na uhaba wa watumishi 15 wa kada tofauti wanaohitajika kutoa huduma hizo.

**HALI YA WATUMISHI WA AFYA - MKOA**

Mkoa wa Lindi una jumla ya watumishi wa kada ya Afya 1,447sawa na asilimia 32.8% ya watumishi wanaohitajika kulingana na ikama ya wizara ya afya ya mwaka 2014 ambao ni 4417. Mkoa unakabiliwa na upungufu wa watumishi wa kada tofauti tofauti za afya kwa asilimia 67.2%. Aidha, ongezeko la upungufu wa watumishi wa afya limeongezeka baada zoezi la uhakiki wa vyeti vya taaluma na masomo kwa watumishi wa umma. Katika mkoa wa Lindi watumishi 244 wa afya walilazimika kuodolewa katika ajira serikalini.

**SEKTA YA MAJI**

**HALI YA UTOAJI HUDUMA YA MAJI VIJIJINI**

Hadi mwezi Juni, 2017 wakazi wapatao 386,866 wanakadiriwa kupata huduma ya maji sawa na 52.3% ya wakazi wote waishio vijijini. Jumla ya vituo vya kuchotea maji vinavyofanya kazi ni 1,700.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, kiasi cha TSh. 6,311,575,000/= kilitengwa kwenye bajeti za Halmashauri za Mkoa wa Lindi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Katika kiasi hiki, fedha za ndani zilikuwa Tsh. 4,520,435,000 na fedha za nje Tsh. 1,791,139,000. Hadi kufikia Juni 2017 kiasi cha Tsh. 7,214,330,614 kilikuwa kimetolewa kwa ajili ya kulipia madeni ya wakandarasi wa ujenzi wa miradi ya Maji.

Kwa mwaka wa fedha 2017/18 kiasi cha TSH. 6,016,665,000 kimetengwa katika bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Halmashauri za Mkoa wa Lindi kama inavyooneshwa katika jedwali namba 3.

**JEDWALI NA 3: FEDHA ZILIZOTENGWA KWA AJILI YA BAJETI YA MAJI 2017/2018**

| Halmashauri | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kilwa | 1,088,347,000 | 225,719,000 | 1,314,066,000 |
| Lindi | 584,272,000 | 249,593,000 | 833,865,000 |
| Lindi | 862,096,000 | 214,769,000 | 1,076,865,000 |
| Liwale | 453,167,000 | 122,779,000 | 575,946,000 |
| Nachingwea | 453,167,000 | 132,441,000 | 585,608,000 |
| Ruangwa | 1,359,501,000 | 270,814,000 | 1,630,315,000 |
| | **4,800,550,000** | **1,216,115,000** | **6,016,665,000** |

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI KATIKA HALMASHAURI ZA MKOA WA LINDI

Jumla ya miradi 54 katika halmashauri za mkoa wa Lindi ilipangwa kujengwa, kati ya miradi hiyo miradi 39 ni miradi ya vijiji 10. Hadi kufikia mwezi Juni, 2017 miradi 35 ya vijiji 10 imekamilika na miradi 4 iko katika hatua za mwisho za kukamilishwa. Miradi hii ni Nyangamara na Namangare katika halmashauri ya wilaya ya Lindi, Mbekenyela katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na mradi wa maji wa Mkanga katika halmashauri ya manispaa ya Lindi.

Katika kuhakikisha miradi ya maji inakuwa endelevu, miradi yote inaendeshwa na wananchi wenyewe kupitia vyombo huru vya watumiaji maji/vikundi vinavyoundwa kisheria. Hadi kufikia Juni 2017, jumla ya vyombo vya watumiaji 114 vimeundwa na kusajiliwa.

## HALI YA UTOAJI HUDUMA KATIKA MIJI YA WILAYA NA MANISPAA YA LINDI.

Kiwango cha huduma ya maji kwa miji ya makao makuu ya mkoa na wilaya inakadiriwa kuwa wastani wa 56.9%. Katika manispaa ya Lindi, mahitaji ya maji kwa siku ni mita za ujazo 5400. Uwezo wa sasa wa uzalishaji wa maji ni sawa na wastani wa mita za ujazo 940.29 ambayo ni sawa na asilimia 17.41 ya mahitaji halisi. Hali hiyo ya uzalishaji imeonekana kupungua sana kutokana na kusitishiwa huduma ya umeme katika vyanzo vyetu vya Mbanja, Kitunda na Sinde tokea mwezi wa saba mwishoni kutokana na deni la bili ya umeme Tsh. 130,000,000.

Hatua zilizochukuliwa ni kuiandikia Wizara ya Maji na Umwagiliaji ambayo tokea mwanzo ndiyo ilikuwa ikitulipia ankara za umeme. Wizara ya Maji imeomba fedha kutoka hazina ili kulipia deni hili pamoja na madeni ya mamlaka nyingine za maji. Malipo hayo bado hayajatolewa.

## MRADI WA MAJI WA NG`APA

Sote tunatambua kuwa mradi huu umechelewa kukamilika kutokana na kasi ndogo ya mkandarasi. Kutokana na hali hii Wizara ya Maji na Umwagiliaji ililazimika kuweka wataalamu wa kumsimamia mkandarasi na kuhakikisha kuwa anafanya kazi za kipaumbele ambazo zitasaidia kufikisha maji kwenye matanki.

Hadi tunatoa taarifa hii, visima 5 kati ya 8 vinafanya kazi, Machujio yaliyopo Ng'apa yanafanya kazi, Matanki mawili ya Angaza na Cheleweni yameshaweza kupokea maji kutoka Ng'apa.

## HATUA ZINAZOENDELEA; -

Maunganisho ya Matanki ya RIPS, RAS, Wailes na Green yameshafanyika. Utaratibu wa kuingiza maji katika matanki hayo unaendelea na maji hayo yanasambazwa kwa wananchi. Kazi ya kuunganisha matanki ya Jamhuri na Old Mtanda yanaendelea. Maeneo yanayopata maji ya Ngapa kwa sasa ni pamoja na eneo la Kata ya Mwenge katika Mtaa wa Kilimahewa ndipo palipojengwa vituo vya umma 11 ambapo vituo 8 vinaendela kutoa huduma ya maji kwa masaa 24.

Maeneo yanayohudumiwa na Matanki ya RIPS, RAS, Wailesi na Green yataanza kupata maji rasmi na kwa ratiba inayoeleweka, mara majaribio yanayoendelea kukamilika. Kwa sasa huwa yanapata huduma ya maji pindi yanapoingizwa maji kutoka tanki la Angaza au Cheleweni kwa majaribio.

# SEKTA YA KILIMO

## UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA MSIMU WA MWAKA 2016/2017

Mkoa wa Lindi umekamilisha hatua za mavuno kwa msimu huu 2016/2017 isipokuwa kwa mazao ya muhogo na mbaazi. Jumla ya hekta 439,561 zilitarajiwa kulimwa katika wilaya zote

tano (5) kwa halmashauri zote sita. Eneo hilo linatarajia kuzalisha jumla ya tani 603,531 za mazao ya chakula yakiwemo yale ya asili ya wanga na jamii ya mikunde. Kati ya hekta zilizolengwa kulimwa mazao ya chakula; hekta 363,273 ni za mazao ya jamii ya wanga yakiwemo muhogo hekta 103,393; mtama hekta 68,257; mahindi hekta 138,743; mpunga hekta 47,486 na viazi vitamu hekta 5,394. Hekta 76,288 ni za mazao ya jamii ya kunde zikiwemo hekta 47,281 za mbaazi na hekta 29,007 za kunde.

Mkoa umevuna jumla ya tani 439,990 za mazao ya jamii ya wanga yakiwemo muhogo tani 222,114; mtama tani 48,087, mahindi tani 131,871, mpunga tani 29,689 na viazi vitamu tani 8,229. Aidha, jumla ya tani 62,603 za mazao ya jamii ya kunde zinatarajiwa kuvunwa zikiwemo tani 14,955 kwa zao la kunde na tani 30,408 za mbaazi.

## HALI YA CHAKULA

Hali ya chakula kwa sasa ni ya kuridhisha kwenye Halmashauri zote za mkoa wa Lindi. Upatikanaji wa chakula katika mkoa wetu unaridhisha, uvunaji wa mazao mbalimbali umekamilika, isipokuwa kwa mazao ya muhogo na mbaazi ambapo uvunaji unaendelea na matarajio yetu ni kuwa na utoshelevu wa chakula.

## UZALISHAJI WA MAZAO YA BIASHARA MSIMU WA MWAKA 2016/2017

Jumla ya kilo 69,851,740 za korosho zenye thamani ya Tshs. 199,584,635 zimezalishwa, kilo 34,034,000 za ufuta zimezalishwa pia.

Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2015/2016 Mkoa wa Lindi ulipokea jumla ya Tshs. 748,000,000/= kutoka katika mfuko wa kuendeleza miradi ya umwagiliaji (*Small Scale Irrigation Development Programme*) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mtawango uliopo wilaya ya Liwale na Nanganga uliopo wilaya ya Ruangwa. Mpaka kufikia mwisho wa mwaka 2016/2017 utekelezaji wa miradi hii bado haujakamilika ambapo ujenzi wa miundombinu na usanifu unaendelea kama inavyoonyesha kwenye jedwali.

## JEDWALI NA 4: UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UMWAGILIAJI

| Wilaya | Mradi | Eneo Ha | BAJETI 2015/16 | Kazi zilizofanyika | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| Liwale | Mtawango | 230 | 344,000,000 | Kuchimba na kujenga mita 800 za mfereji mkuu kati ya mita 1,400, kufyeka na kusafisha barabara mita 400 ya kuelekea eneo la mradi bado | Mradi unatekelezwa kwa fedha za bakaa ya mwaka 2015/2016 |
| Ruangwa | Nanganga | 250 | 404,000,000 | Usanifu wa mradi bado unaendelea | Mradi unatekelezwa kwa fedha za bakaa ya mwaka 2015/2016 |

### Changamoto

Kilimo cha umwagiliaji kimekuwa kinakumbwa na changamoto mbalimbali miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na eneo kubwa linalofaa kwa shughuli za umwagiliaji halijaendelezwa kutokana na ukosefu wa fedha. Kwa sasa eneo linalomwagiliwa ni hekta 2,010 kati ya hekta 10,000 zinazofaa kwa kilmo cha umwagiliaji, na mwamko mdogo wa wakulima kujihusisha na kilimo cha umwagiliaji.

## ZANA ZA KILIMO

Mkoa una trekta kubwa 154, Power Tiller 385, na jozi za maksai 262. Hali ya zana kwa kila Halmashauri imeonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Katika msimu wa kilimo mwaka 2016/2017 jumla ya hekta 21,682 zililimwa kwa kutumia trekta na hekta 1,192 zililimwa kwa kutumia majembe ya kukokotwa na wanyama kazi sawa na 3.3% ya eneo lote linalolimwa.

**JEDWALI NA 5 AINA NA IDADI YA ZANA ZA KILIMO**

| HALMSHAURI | TREKTA | NZIMA | MBOVU | POWERTILLER | NZIMA | MBOVU | JOZI ZA MAKSAI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| LINDI | 29 | 24 | 5 | 112 | 7 | 105 | 62 |
| LINDI MANISPAA | 16 | 14 | 2 | 19 | 0 | 19 | 0 |
| KILWA | 13 | 9 | 4 | 61 | 2 | 59 | 144 |
| LIWALE | 20 | 16 | 4 | 43 | 27 | 16 | 30 |
| NACHINGWEA | 60 | 45 | 15 | 24 | 0 | 24 | 18 |
| RUANGWA | 25 | 21 | 4 | 94 | 77 | 17 | 8 |
| **JUMLA** | **154** | **125** | **29** | **385** | **175** | **210** | **262** |

**MIKAKATI WA MKOA KATIKA KUONGEZA TIJA KWA KUTUMIA ZANA BORA ZA KILIMO**

Ili kuboresha kilimo na kuongeza tija katika kutumia zana bora za kisasa mkoa umekuwa ukifanya mambo yafuatayo: -

i. Kuendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya umuhimu wa kuongeza matumizi ya zana za kilimo pamoja na kufuata kanuni bora za kilimo.

ii. Kuendelea kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa karibu juu ya kanuni za kilimo cha kisasa ili kuongeza tija.

iii. Kwa kushirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya mkoa, kuendelea kuhamasisha kuanzishwa kwa karakana/maduka ya vifaa na spea za zana za kilimo.

iv. Kuendelea kuzisimamia halmashauri ili ziweze kufanya mafunzo ya wagani, ambao watapatiwa mafunzo ya kilimo cha kisasa pamoja na matumizi ya zana bora za kilimo ili nao waweze kuwafundisha wakulima wenzao katika vijiji wanakotoka, hii ikiwa moja ya njia ya kupambana na upungufu wa maafisa kilimo.

v. Mkoa kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo kendelea kuwahimiza wakulima kuomba mikopo kutoka katika taasisi za fedha ili kuwawezesha kujinunulia zana bora za kilimo (kwa mfano dirisha la kilimo-TIB na TADB).

**JEDWALI NA 6: CHANGAMOTO NA MIKAKATI**

| Na. | CHANGAMOTO | MIKAKATI |
|---|---|---|
| 1. | Uwepo wa visiki katika mashamba yaliyo mengi hivyo kukwamisha matumizi ya matrekta. | Kuwahamasisha wakulima kuondoa visiki katika mashamba yao ili eneo litakalolimwa kwa kutumia matrekta liongezeke. |
| 2. | Uhaba wa vipuli na karakana za trekta kwa ajili ya matengenezo. | Kuendelea kuhamasisha wafanya biashara wa zana za matrekta na vipuli waweze kuanzisha maduka. |
| 3. | Idadi ndogo ya Matrekta | Kuwahamasisha watu binafsi wanunue matrekta madogo na makubwa. |
| 4. | Elimu duni juu ya matumizi ya matrekta. | Kuendelea kutoa elimu ya kilimo cha Matrekta kwa vikundi vinavyomiliki Matrekta, kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Biashara. |

Kwa ujumla hali ya matumizi ya zana bora za kilimo bado yako chini. Asilimia kubwa ya wakulima wanatumia jembe la mkono, hii inatokana na mashamba mengi bado yanavisiki. Hivyo, kadri wakulima wanavyozidi kutoa visiki mashambani mwao, ndivyo watakavyozidi kutumia zana bora za kilimo na hasa matrekta makubwa, na hivyo asilimia ya matumizi ya zana bora yataongezeka, matokeo yake wakulima watapata mavuno mengi.

## HALI YA USHIRIKA HADI KUFIKIA TAREHE 31 AGOSTI, 2017

Mkoa una jumla ya vyama vya ushirika 263 kati ya hivyo, vyama vya Ushirika vya mazao (AMCOS) 137, vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) ni 121, vyama vinginevyo 5. Aidha, kuna vyama vikuu vya ushirika 2 vya RUNALI (kwa ajili ya Halmashauri za Ruangwa, Nachingwea na Liwale) na LINDI MWAMBAO (kwa halmashauri za Kilwa, Lindi na Manispaa ya Lindi). Usajili wa vyama hivi umekamilika tangu mwezi Aprili, 2017.

## UANDIKISHA WA AMCOS, SACCOS NA VYAMA VINGINEVYO

Hali ya uandikishaji wa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS), Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) na vyama vinginevyo kwa mwaka wa 2016/2017 ilikuwa kama ifuatavyo: -

## JEDWALI NA 7: UANDIKISHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA

| AINA YA CHAMA | MALENGO | VILIVYOSAJILIWA | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| AMCOS | Vyama 10 | 6 | Vimekidhi sifa na uwezo wa kisheria |
| SACCOS | Vyama 5 | 2 | Vimekidhi sifa na uwezo wa kisheria |
| Vyama Vinginevyo | Vyama 3 | 0 | Uhamasishaji unaendelea. Chama cha Ushirika tarajiwa wa madini kimeanza mchakato wa awali |
| **Jumla** | **Vyama 18** | **Vyama 8** | |

## USAJILI WA VYAMA VIKUU VYA RUNALI NA LINDI MWAMBAO LTD:

Vyama vikuu vya ushirika viwili – LINDI MWAMBAO na RUNALI vimeandikishwa kisheria chini ya matazamio ya miaka miwili. Mrajis wa vyama vya ushirika ametoa maelekezo kwa bodi anzilishi kusimamia maendeleo ya vyama hivyo vikuu na kuhakikisha kuwa masharti waliopewa yakiwemo uhamasishaji uandikishaji wa wanachama na utoaji wa hisa unakamilika Agosti, 2017. Vyama vikuu wameviandikia vyama vya ushirika vya msingi barua kuvitaka kutimiza wajibu wao wa kisheria kama Mrajis alivyoelekeza ili viweze kukidhi sifa za kisheria kupata usajili wa kudumu. Vyama vya ushirika vya msingi vimehamasika na vinasubiri kupewa akaunti maalum kwa ajili ya kulipia ada ya kiingilio na hisa stahiki.

Shughuli zinazoendelea kufanyika hivi sasa ni pamoja na utoaji wa elimu kwa viongozi wapya wa vyama vya ushirika vya msingi juu ya haki na wajibu wa viongozi katika usimamizi wa vyama vyao, uhamasishaji wakulima kuendelea kutumia pembejeo zilizohakikiwa na mamlaka husika ili mavuno yaweze kutoa korosho zilizo bora na uhamasishaji wakulima kuendelea kufungua akaunti benki.

## UFILISI WA KILICHOKUWA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA ILULU

Kazi ya uhakiki wa mali zilizopo na maeneo ambayo mali hizi zipo umefanyika (Physical stock taking), uhakiki wa madeni kulingana na taarifa ya ukaguzi wa hali ya taasisi iliyofanywa na COASCO na ufuatiliaji wa madeni hayo kutoka kwa wadeni ambao hadi sasa yana thamani ya shilingi bilioni 13 umefanyika.

Aidha, ufuatiliaji wa kesi zilizokuwa mahakamani ambapo wadai walikuwa wakamate mali za ILULU kwa ajili ya kuziuza na juhudi zimefanyika kushinda rufaa iliyowataka wadeni kudai kama wadai wengine, pia uthamini upya wa mali za Ilulu umefanyika. Jitihada zinaendelea za kusubiri taarifa ya mthamini mkuu wa Serikali. Vilevile uthamini wa mwisho unaonesha mali zilizopo zina thamani ya shilingi 558,727,300.

**UKAGUZI WA VYAMA VYA USHIRIKA**:

Ukaguzi wa vyama vya ushirika ni muhimu kwa wanachama kuelewa maendeleo ya chama chao kiuchumi kutokana na usimamizi wa wajumbe wa bodi pamoja na utendaji wa watumishi wao. Hadi kufikia mwaka huu wa 2016/2017 hali ya ukaguzi ilikuwa kama ifuatavyo: -

**JEDWALI NA 8: HALI YA UKAGUZI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA:**

| AINA YA CHAMA | IDADI | MALENGO | VILIVYOKAGULIWA | MKAGUZI |
|---|---|---|---|---|
| AMCOS | 107 | 113 | Msimu 2015/2016 vyama 99 vilikaguliwa na AMCOS 14 hazikukaguliwa kutokana na kukosekana kwa vitabu vya hesabu pamoja na viambatisho. | **COASCO** |
| | | 107 | Msimu 2012/2013 vyama 104 | COASCO |
| | | 65 | Msimu 2014/2015 Vyama 21 | Idara ya Ushirika |
| SACCOS | 114 | 110 | Msimu 2015/2016 Vyama 8 | Idara ya Ushirika<br>COASCO |
| | | | Msimu 2012/2013 Vyama 15 | COASCO |
| | | 55 | Msimu 2014/2015 vyama 10 | Idara ya Ushirika |
| CHAMA KIKUU – ILULU | 1 | 1 | Msimu 2013/2015 - | COASCO<br>Idara ya Ushirika |

**UCHAGUZI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA**

Mwaka 2017 ni mwaka wa uchaguzi wa viongozi wa bodi za vyama vya ushirika kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni yake ya mwaka 2015. Katika mkoa wa Lindi, chaguzi zilianza mwezi Mei, 15, 2017. Chaguzi zimekamilika kwa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) vipatavyo 136 kati ya 137. Chama cha ushirika cha msingi SUDI bado hakijafanya mkutano mkuu kutokana na changamoto ya kutomaliza malipo ya korosho ya msimu uliopita kwa wakulima. Uchaguzi wa Viongozi wa SACCOS muda wake ni kuanzia Oktoba, 2017. Aidha, kabla ya mikutano mikuu ya uchaguzi kwa vyama vya ushirika, kulitanguliwa na usomaji wa taarifa za ukaguzi wa COASCO kwa hesabu za msimu 2015/2016 ambapo jumla ya AMCOS zipatazo 66 zilisomewa hesabu na bodi zimewajibishwa kwa kuondolewa madarakani.

**UTATUZI WA MIGOGORO KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA**

Migogoro mingi katika vyama vya ushirika inatokana na wizi wa fedha za wakulima unaofanyika kwenye baadhi ya vyama vya ushirika vya msingi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi Nahukahuka AMCOS – ilipata upotevu wa fedha za mauzo ya korosho ya wakulima Tsh. 76,049,400, juhudi zilizofanyika ni pamoja na:-

- Kuwakamata viongozi na kuwaweka ndani ili wananchi watambue kuwa serikali inawajali na inafuatilia madai yao.
- Kuteua timu ya wajumbe 4 kufanya uchunguzi wa mazingira yaliyosababisha upotevu wa fedha za wakulima. Timu ilijumuisha wajumbe kutoka Tume ya ushirika 1, Mwanasheria ofisi ya Katibu Tawala Mkoa 1, Mkurugenzi wa halmashauri -1 na LINDI MWAMBAO 1 (Union).
- Taarifa imeandaliwa na imewasilishwa kwa mwanasheria mfawidhi wa serikali kwa hatua zaidi za kisheria ili kuwabana wahusika kuwajibika kurejesha fedha.
- Mwanasheria amekamilisha zoezi la uchambuzi wa taarifa na amewasilisha kwa Mrajis Dodoma ili aweze kuandaa "Surcharge" kwa mujibu wa sheria ya ushirika itakayompa mamlaka ya kuwatia hatiani viongozi.

Aidha, katika chama cha Nanyumu AMCOS ulitokea wizi wa fedha takribani Tsh. milioni **443** msimu 2015/2016 zikiwa ni mauzo ya korosho ya wakulima. Kesi ilipelekwa mahakamani na watuhumiwa walishinda. Serikali chini ya mwanasheria mfawidhi wa Serikali kanda ya Lindi imekata rufaa hivyo kinachosubiriwa ni wito wa mahakama ili kesi hiyo isikilizwe upya.

Kumekuwa na malalamiko ya wakulima kutolipwa fedha zao za mauzo ya korosho msimu wa 2016/2017 katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale AMCOS 3 ambazo hazijamaliza kulipa wakulima ni Nambana AMCOS Tsh. 36,765,650, Mikunya AMCOS Tsh. 29,078,670, Mahonga AMCOS Tsh. 33,800,000.

Mwenendo wa kesi zilizopo mahakamani zipo katika hatua ya upelelezi na mpaka sasa taarifa za ukaguzi za COASCO kwa vyama vya ushirika 2 ambavyo havikukamilisha malipo kwa wakulima tayari zimewasili, bado chama cha ushirika 1. Taarifa za ukaguzi zilizowasili Polisi kutoka COASCO ni za chama cha Ushirika cha Mazao NAMBANA na MIKUNYA bado MAHONGA AMCOS. Utaratibu wa COASCO kuja kukamilisha Ukaguzi wa Chama cha Msingi MAHONGA umekamilika. Ukaguzi unaanza tarehe 04 Septemba, 2017.

Chama cha Sudi AMCOS kiliuza kilo 994,970 zenye thamani ya Tshs. 3,537,882,875. Malipo yaliyofanyika kwa wakulima ni 3,450,338,132. Bado kukamilisha kwa malipo ya wakulima wa matawi matatu (3) ambayo ni Madangwa, SUDI na Mtegu. Madai ya awali ya wakulima yalikuwa Tshs. 87,544,743 kwa mchanganuo ufuatao Sudi wakulima 8 Tshs 15,646,848, tawila Madangwa wakulima 16 Tshs. 60,064,383, tawil la Mtegu – wakulima 5 Tshs. 11,833,512, Wakulima wanadai Tshs. 92,354,213 na hatua iliyochukuliwa Bodi iliandikiwa barua kuwajibika juu ya upungufu wa mazao uliotokea wastani wa kilo 22,016,018.

Halmashauri ya wilaya ya Kilwa Urina AMCOS jumla ya madai ya awali yalikuwa ni Tshs. 121,188,691.87. Malipo yameendelea kufanyika kwa wakulima kila baada ya kupokea marejesho kutoka kwa wakulima walioingiziwa fedha kwenye akaunti zao kimakosa. Jumla ya malipo yaliyofanyika ni Tshs. 37,198,220.98. Ofisi ya Mrajis Dodoma imefanya ukaguzi mwezi Agosti, 2017 kuhakiki madai halisi hadi sasa. Taarifa inaandaliwa.

Pia kuna vyama vinavyotaka kujigawa na kujitenga katika wilaya ya Nachingwea. Vyama hivyo ni NAIPANGA na MTUA AMCOS.

**UPATIKANAJI WA PEMBEJEO**

Mkoa wa Lindi ulipangiwa kupokea mgao wa jumla ya kilo 4,108,745 za salfa ya unga, lita 75,327 za dawa za maji pamoja na mabomba 336. Mpaka sasa mkoa umepokea jumla ya kilo 3,871,904 sawa na asilimia 94.24% na tayari zimeshasambazwa. Kwa upande wa viatilifu vya maji mkoa umepokea lita 75,737, sawa na asilimia 100%. Mpaka sasa mkoa umepokea mabomba yote 336 na kuyasambaza kwa wakulima.

## MAONESHO YA NANE NANE KITAIFA KWA MWAKA 2017

Maonesho ya Nane nane kitaifa katika kanda ya kusini yalifanyika kwa mwaka wa nne mfululizo katika viwanja vya Ngongo – Manispaa ya Lindi kuanzia tarehe 1-8/8/2017. Katika kipindi chote hicho mikoa ya Lindi na Mtwara imeratibu vema na kufanikisha kufanyika maonesho haya. Mafanikio haya yalitokana na kujitokeza kwa wingi kwa taasisi mbalimbali ambazo zimeshiriki pamoja na kutoa michango yao ya hali na mali. Aidha, mafanikio mbalimbali ya kuwepo kwa Nane nane kitaifa katika mkoa wa Lindi yanazidi kuonekana ikiwemo kuendelea kuboreka kwa miundombinu ya barabara na majengo katika maeneo ya viwanja vya Nane nane Ngongo na wakulima kupata fursa ya kujifunza teknolojia mpya ya kilimo cha biashara.

Pamoja na mafanikio hayo kwa upande wa wakulima maonesho hayo yamewezesha kupanuka kwa fursa za biashara kwa watoa huduma za kibiashara hususani nyumba za kulala wageni, migahawa, wauzaji vyakula, vinywaji na usafirishaji. Kwa mwaka huu maandalizi yamekuwa ya kuridhisha kwa upande wa upandaji wa vipando mbalimbali katika maeneo ya halmashauri na taasisi zote za umma na binafsi kutoka kanda ya kusini na Tanzania kwa ujumla. Kaulimbiu ya Nanenane 2017 ilikuwa ***"Zalisha kwa tija mazao na bidhaa za kilimo, mifugo na uvuvi ili kufikia uchumi wa kati".***

## SEKTA YA NISHATI

### HALI YA UMEME

Mkoa wa Lindi unapata umeme kutoka katika kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia kilichoko Mtwara kwa wilaya za Ruangwa, Nachingwea na sehemu ya Kilwa, Lindi mjini na vijijini. Wilaya ya Kilwa inapata umeme kutoka kituo cha kuzalisha umeme kinachotumia gesi asilia kilichoko Somanga na wilaya ya Liwale inapata umeme kutoka katika kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia dizeli kilichopo Liwale. Kwa sasa shirika la umeme lina jumla ya wateja 28,402.

### MIRADI YA UBORESHAJI WA HALI YA UMEME MKOA WA LINDI.

Shirika la Umeme Lindi limekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolti 132 kutoka Mtwara hadi Mahumbika Lindi yenye urefu 80km na kujenga kituo cha kuongeza nguvu umeme chenye ukubwa wa 20MVA, 33/132kV kilichopo mkoani Mtwara na kile cha kupoza nguvu ya umeme chenye ukubwa wa 20MVA, 132/33kV kilichopo Kijiji cha Mahumbika mkoani Lindi. Ujenzi wa njia mbili mpya za msongo wa kilovoti 33 zenye urefu wa 31km, zinazosambaza umeme maeneo ya Lindi mjini, na njia ya kuelekea wilaya ya Kilwa inayosambaza umeme maeneo yaliyo ndani ya Lindi na baadhi ya sehemu ya wilaya ya Kilwa.

Utekelezaji huu umelenga kuboresha upatikanaji umeme na kuhakisha kuwa Mkoa wa Lindi unakuwa na umeme wa uhakika na hatimaye kuwa sehemu kubwa ya kichocheo kuelekea Tanzania ya viwanda.

### UTEKELEZAJI WA MIRADI YA REA

Katika mkoa wa Lindi jumla ya vijiji 120 vilipata umeme kupitia miradi ya umeme vijijini awamu ya pili (REA Phase II projects). Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani tarehe 18/8/2017 katika kijiji cha Chinongwe Ruangwa alizindua awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu kwa Mkoa wa Lindi ambao unahusisha upelekaji umeme katika vijiji 133 kwa gharama ya Tshs. 31.60 Bilioni.

## SEKTA YA MADINI

## AINA YA MADINI YANAYOPATIKANA LINDI

Sekta ya madini ni sekta inayoanza kukua kwa kasi katika mkoa wetu pamoja na kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoikabili kama ukosefu wa miundombinu ya barabara, maji, huduma za jamii na umeme wa uhakika katika maeneo madini yanapopatika. Kukua huku kumetokana na usimamizi mzuri wa mkoa kwa kushirikiana na kamishna wa madini, wananchi, wadau na uwepo wa madini ya aina mbalimbali, kukua kwa teknolojia na uwepo wa wawekezaji wakubwa na wadogo katika sekta hii.

Katika mkoa wa Lindi madini yapo katika wilaya zote kama ifuatavyo : -

- Wilaya ya Lindi ina madini ya ujenzi, chumvi, mawe ya chokaa, feldspar, pozzolana, Makaa ya mawe, chuma, jasi (gypsum) na kinywe (graphite).
- Wilaya ya Kilwa ina madini ya jasi (gypsum), mawe ya chokaa, madini ya ujenzi, chuma, vito na kinywe (graphite).
- Wilaya ya Ruangwa ina madini ya dhahabu, vito, kinywe (graphite), madini ya ujenzi, chuma, shaba na feldspar.
- Wilaya ya Liwale ina madini ya dhahabu, nikeli, mabo (marble), manganese na amazonite.
- Wilaya ya Nachingwea ina madini ya dhahabu, kinywe (graphite), vito, chuma, shaba na Nikeli.

## LESENI ZA UTAFITI (PLs)

Leseni ya utafiti (Prospecting Licence), ina uhai wa miaka 4, ikihuishwa mara ya kwanza miaka 3, ikihuishwa mara ya pili miaka 2. Leseni hii hutolewa na Kamishna wa Madini, DSM. Kiwango cha juu cha ukubwa wa leseni hizi na kilometa za mraba 300 (50% relinquishment). Leseni ya utafiti ya Vito isipokuwa almasi: Ina uhai wa mwaka mmoja na haihuishwi. Leseni hii hutolewa na Kamishna wa Madini, DSM. Ukubwa usiozidi kilometa za mraba 5.

Leseni ya Utafiti wa madini ya ujenzi: Ina uhai wa mwaka mmoja na haihuishwi. Leseni hii hutolewa na Kamishna wa Madini, DSM. Ukubwa usiozidi kilometa za mraba 5. Leseni ya kuhodhi eneo (Retention Licence): Leseni ni ya miaka mitano na inaweza kuhuishwa kwa miaka mingine mitano. Leseni hii hutolewa na Waziri wa Nishati na Madini endapo hali ya uchumi hairuhusu kuanza uchimbaji katika eneo lililofanyiwa utafiti.

## LESENI ZA UCHIMBAJI MADINI

Leseni ya uchimbaji wa kati (ML), hutolewa kwa miaka 10 na inahuishwa kwa miaka mingine 10. Hutolewa na Waziri wa Nishati na Madini. Ukubwa usiozidi kilometa za mraba 10. Leseni Kubwa ya uchimbaji Madini (SML): Hutolewa kwa miaka 25 na inahuishwa kwa miaka mingine 25. Hutolewa na Waziri wa Nishati na Madini. Ukubwa usiozidi kilometa za 35 kwa madini ya kwenye miamba na usiozidi kilometa za mraba 70 kwa madini ya tabaka lilitokana na kusagika kwa miamba (superficial deposit).

Uchimbaji mdogo wa madini (PMLs) Leseni za uchimbaji mdogo wa madini (PMLs): Zina uhai wa miaka 7 kwa madini yenye uchimbaji wa muda mrefu (zina ukubwa wa hekta 10) na mwaka mmoja kwa leseni leseni zenye uhai mfupi mfano mchanga na kifusi (zina ukubwa wa hekta 5 kiwango cha juu). Hizi ni kwa Watanzania tu. Zinahuishwa kwa miaka mingine saba na huombwa upya kwa zile za mwaka mmoja. Leseni hizi hutolewa na Afisa Madini Kanda.

**UCHENJUAJI WA MADINI**

Leseni za kuchenjua madini (Processing Licence): Hutolewa na Kamishna wa Madini na zina uhai wa miaka 10 na zinahuishwa kwa kipindi kingine cha miaka 10. Leseni za kuyeyusha/Kuchoma madini (Smelting Licence): Hutolewa na Waziri na zina uhai wa miaka 25 na zinahuishwa. Leseni za kusafisha madini (Refining Licence): Hutolewa na Waziri na zina uhai wa miaka 25, pia zinahuishwa.

**LESENI ZA BIASHARA YA MADINI**

Leseni Kubwa ya Biashara ya Madini (Dealers licence): Hutolewa na Afisa Madini Kanda na huisha tarehe 30/06 ya kila mwaka na huombwa upya. Leseni ndogo ya biashara ya Madini (Broker's licence): Hutolewa na Afisa Madini Kanda na huisha tarehe 30/06 ya kila mwaka na huombwa upya. Hii ni kwa Watanzania tu na haimruhusu mmiliki kuuza madini nje ya nchi. Hadi kufikia Agosti, 2017 jumla ya leseni 2,282 zimetolewa katika mkoa wa Lindi. Taarifa hii pia imewasilishwa kwa wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa wilaya husika kwa ajili ya rejea. Mchanganuo wa leseni hizo umeoneshwa katika jedwali na. 12.

**JEDWALI NA 9: AINA NA IDADI YA LESENI ZILIZO HADI AGOSTI 2017**

| **Eneo/Mahali** | **PMLs** | **PLs** | **MLs** | **SMLs** | **RLs** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Lindi Vijijini | **189**<br>Chumvi, Madini ya Ujenzi, Jasi na madini mengine | **6**<br>Chokaa, Jasi, Kinywe na Madini mengine | - | - | - | 195 |
| Lindi Mjini | **99**<br>Chumvi, Madini ya Ujenzi, Chokaa | **2**<br>Chokaa | **-** | **-** | **-** | 101 |
| Kilwa | **1231**<br>Chumvi, Madini ya Ujenzi, Jasi, Chokaa, Madini Mengine | **22**<br>Dhahabu, Mchanga, Chokaa, Kinywe, Jasi na Madini mengine | **7**<br>Jasi | **-** | **-** | 1260 |
| Ruangwa | **278**<br>Vito, Dhahabu, Kinywe, Shaba, Chuma, Madini ya Ujenzi na Madini mengine | **28**<br>Dhahabu, Shaba, Kinywe, Nikeli | **9**<br>Dhahabu, Kinywe na Vito | **1**<br>Kinywe | **-** | **316** |
| Nachingwea | **156**<br>Vito, Dhahabu, Kinywe, Shaba, Chuma, Madini ya Ujenzi na Madini mengine | **14**<br>Dhahabu, Shaba, Kinywe, Nikeli na Chuma | **1**<br>Vito | - | **1**<br>Nikeli | **172** |

| Eneo/Mahali | PMLs | PLs | MLs | SMLs | RLs | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Liwale | **162**<br>Vito, Dhahabu na Madini mengine | **30**<br>Dhahabu, Manganese, Uranium na Nikeli | **2**<br>Dhahabu | - | - | **194** |
| Zinazoingiliana Mpika ya Wilaya za Lindi na baadhi Mtwara | - | **44**<br>Jasi, Dhahabu, Nikeli, Shaba, Kinywe, Chokaa, Makaa ya Mawe na Madini mengine | - | - | - | **44** |
| Jumla1 | **2115** | **146** | **19** | **1** | **1** | **2282** |

Mkoa umeendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za madini kwa kushirikiana na kamishna wa kanda wa madini pamoja na wadau katika kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidiaka na uwepo wa madini haya na wanashirikishwa katika hatua zote za uanzishwaji na uchimbaji wa madini katika maeneo yao.

**SEKTA YA BARABARA**

Mkoa wa Lindi una mtandao wa barabara wenye urefu wa km 1,293.28 ambazo zinahudumiwa na Wakala wa barabara. Mtandao huu umegawanyika katika barabara kuu (Trunk Roads) zenye urefu wa km 348.12 na barabara za mkoa (Regional Roads) zina jumla ya urefu wa km 945.16. Km 348.12 zote za barabara kuu ziko kwenye kiwango cha lami na katika barabara za mkoa ni km 36 pekee ndiyo ziko kwenye kiwango cha lami.

**HALI YA BARABARA**

Kwa kifupi barabara zote za mkoa wa Lindi kwa sasa ziko katika hali nzuri na zinapitika vizuri baada ya matengenezo yaliyofanyika kwa ufanisi wakati wa mvua za msimu.

**MATENGENEZO YA BARABARA**

Katika mwaka wa fedha 2016/17, mkoa wa Lindi ulitengewa jumla ya shilingi 14,665.710 milioni kutoka mfuko wa barabara (Roads Fund) kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mkoa pamoja na madaraja. Kutokana na mapungufu ya fedha kwa mwaka wa fedha 2015/16 bajeti hii ilipunguzwa hadi shilingi milioni 9,642.825.

Hadi mwezi Julai, 2017 utekelezaji wa kazi kwa wastani umefikia asilimia 90 na kazi zinazoendelea zipo katika barabara zifuatazo, Mtegu – Mingoyo 80%, Malendego – Nangurukuru 70%, Nangurukuru – K/Masoko 80%, Nanganga – Nachingwea 70%, Nachingwea – Liwale 75% na Liwale – Nangurukuru (Mlima Tembo) 75%. Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (200KM) upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ulikamilika mwaka 2014 kwa ajili ya kuifanyia ukarabati (Rehabilitation) kwa kiwango cha lami. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi (Ukarabati).

Barabara ya Masasi – Nachingwea – Nanganga (KM 91) upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami ulianza Machi, 2013 na kukamilika Agosti, 2014. Nyaraka za zabuni zilishawasilishwa TANROADS Makao Makuu na katika mwaka wa fedha 2017-18 jumla ya shilingi milioni 3,515.394 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Ujenzi daraja la Nandanga (Barabara ya Luchelegwa – Ndanda). Fedha kwa ajili ya usanifu wa mradi huu zilianza kutengwa mwaka wa fedha 2013/14. Kazi za usanifu wa daraja zilianza Januari, 2014 na kukamilika Julai, 2014. Kazi za ujenzi wa daraja zilianza Mei, 2017 kwa mkataba wa jumla ya shilingi milioni 5,409.8 na zinatarajiwa kukamilika Novemba, 2018.

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Nanganga - Ruangwa (KM 60) na Nachingwea – Makanjiro – Ruangwa (KM 44) ulifanyika kufuatia ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyoitoa mwaka 2015 ya kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilitenga shilingi milioni 500 na shilingi milioni 300 kwa mwaka wa fedha 2017-18 kwa ajili ya kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Mkataba wa mhandisi mshauri ulisainiwa tarehe 10/2/2017 na tayari mhandisi mshauri ameanza kazi na kazi zitakamilika Aprili, 2018 tayari kwa ujenzi kuanza mwaka wa fedha 2018-19.

Barabara ya Ruangwa – Namichiga - Kiranjeranje (KM 112). Barabara hii imeingizwa katika Mpango Mkakati wa TANROADS (Strategic plan) kwa kipindi cha 2016/17 - 2020/21 kwa ajili ya kufanyiwa Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Ujenzi wa maegesho ya kivuko (Lindi – Kitunda), kazi za ujenzi wa maegesho zilianza mwezi Mei 2017 kwa jumla ya shilingi 1,971,000,000/= zilitengwa na ujenzi inatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2017. Ninayo furaha kukueleza kuwa kazi zinaendelea vizuri kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Ilani ya CCM ya mwaka 2015 uk 59 hadi uk 61 imezitaja barabara zifuatazo kuwa zitafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara ya Kilwa — Liwale - Nachingwea (km 258), barabara ya Liwale – Nachingwea – Ruangwa (km 185). Hata hivyo sehemu ya barabara hii ya Nachingwea – Ruangwa (km 44) tayari upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeanza katika mwaka 2016/17 pamoja na sehemu ya Ruangwa – Nanganga (60 km).

## MAENDELEO YA SEKTA YA ARDHI MWAKA 2016/2017

Mkoa umeendelea kusimamia mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji pamoja na mipango kabambe ya miji. Katika mwaka 2016/2017 jumla ya vijiji 164 (ikiwa ni asilimia 33 ya vijiji vyote 536 vya mkoa wa Lindi) vilikua na mipango ya matumizi bora ya ardhi.

## MASHAMBA MAKUBWA.

Mkoa wa Lindi una jumla ya mashamba makubwa mia moja thelathini na sita (136). Kati ya mashamba hayo mashamba 60 yameendelezwa, mashamba 76 hayajaendelezwa, mashamba 56 yametelekezwa, mashamba 6 yamerudishwa (surrender) na mashamba 14 yamefutiwa miliki zake za ardhi. Baadhi ya mashamba hayo yanalipiwa kodi na baadhi ya mashamba yamevamiwa na wananchi.

Katika kipindi cha 2016/2017 kazi iliyofanyika ilikuwa ni pamoja na;

i. Kufanya ukaguzi katika mashamba hayo na kuendelea kuandaa taarifa ya orodha ya mashamba, mali zilizomo na ukubwa wa maeneo yaliyovamiwa.

ii. Kutoa ilani za kusudio la kufuta miliki za mashamba yasiyoendelezwa,

Kwa mwaka 2016/2017 halmashauri ya manispaa na halmashauri za wilaya ziliandaa na kutuma jumla ya ilani 49 za kusudio la kufuta miliki za mashamba makubwa yasiyoendelezwa.

**UPIMAJI WA ARDHI NA VIWANJA.**

Kwa mwaka 2016/2017 halmashauri ya manispaa ilipima viwanja 6,200 katika maeneo ya Ngongo, Mnazi mmoja, Mpilipili na Kariakoo. Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea ilipima viwanja 800 vikiwa ni mpango wa kurekebisha makazi mjini. Halmashauri ya wilaya ya Liwale imepima viwanja 500. Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa imetenga eneo la ekari 100 kwa ajili ya upimaji viwanja na tayari fidia imelipwa katika eneo la ekari 10.

**UANDAAJI HATIMILIKI ZA VIWANJA NA HAKIMILIKI ZA KIMILA**

Mwaka 2016/2017 halmashauri za wilaya ziliandaa hati za hakimiliki za kimila 986 na halmashauri ya manispaa na halmashauri za wilaya ziliandaa hatimiliki za viwanja 1,585 kama ilivyofafanuliwa katika jedwali hapo chini.

**JEDWALI 10. HATI ZA HAKIMILIKI ZA KIMILA NA HATIMILIKI ZA VIWANJA.**

| **Halmashauri** | **Hakimiliki za kimila** | **Hati miliki za Viwanja** | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Malengo** | **Utekelezaji** | **Asilimia** |
| Lindi Manispaa | - | 6,700 | 1,014 | 15.3 |
| Kilwa | 53 | 2,500 | 229 | 9.16 |
| Liwale | - | 2,000 | 187 | 9.36 |
| Ruangwa | - | 250 | 95 | 38 |
| Lindi | 33 | 150 | 8 | 1.6 |
| Nachingwea | 903 | 2,500 | 52 | 2.05 |
| **Jumla** | **986** | **14,100** | **1,585** | **11.24** |

**UKUSANYAJI WA MADUHULI YA SERIKALI NA KODI ZAVIWANJA.**

Kwa mwaka 2016/2017 mkoa ulikuwa na lengo la kukusanya Tsh. 3,270,000,000 kama maduhuli na kodi za ardhi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2017 halmashauri za wilaya na manispaa zilikuwa zimekusanya jumla ya Tsh. 2,819,412,136, ikiwa ni asilimia 86 ya lengo la makusanyo kwa mwaka kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo chini.

**JEDWALI Na. 11: UKUSANYAJI WA KODI ZA ARDHI 2016/2017**

| **HALMASHAURI** | **LENGO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
|---|---|---|---|
| Lindi Manispaa | 1,500,000,000 | 627,294,123 | 42. |
| Lindi | 170,000,000 | 135,612,130 | 80. |
| Kilwa | 1,200,000,000 | 1,809,244,744 | 152. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ruangwa | 70,000,000 | 51,861,873 | 74. |
| Nachingwea | 180,000,000 | 86,706,222 | 48. |
| Liwale | 150,000,000 | 106,693,044 | 71. |
| **Jumla Kuu** | **3,270,000,000** | **2,819,412,136** | **86.** |

**MAENEO YA UWEKEZAJI KATIKA ARDHI.**

Mkoa wa Lindi unaendelea kupokea wawekezaji wadogo wakati na wakubwa. Wawekezaji hao wanahitaji ardhi, hadi kufikia mwaka 2016/2017 wawekezaji wakubwa 7 walionesha nia ya kuwekeza katika ardhi. Endapo uwekezaji huo utakamilika utachangia upatikanaji wa ajira, ongezeko la kipato na hatimaye kupunguzaji umaskini kwa kiasi kikubwa. Wawekezaji hawa wanataka kuwekeza katika maeneo ya viwanda vya kuchakata gesi asilia, madini ya kinywe, na viwanda vya mihogo na mbolea.

**JEDWALI Na. 12: UWEKEZAJI KATIKA ARDHI.**

| Kampuni ya Uwekezaji | Mahali anapowekeza. | Matumizi ya ardhi | Ukubwa (ha.) | Hali halisi |
|---|---|---|---|---|
| Cassava Starch of Tanzania Corporation Ltd. | Wilaya ya Lindi. Vijiji 6 vya Linoha, Mandwanga, Lipome, Nahukahuka A na B na Lindwandwali. | Kilimo cha Mihogo | 3,004.1 | Uthamini katika vijiji vya Lipome, Linoha Lindwandwali, na Nahukahuka B tayari. Fidia imelipwa katika vijiji vya Lipome na Lindwandwali. |
| Uranex Tz, Ltd. | Wilaya - Ruangwa. Vijiji sita 6 vya Mradi ya machimbo kinywe. | Machimbo ya madini ya kinywe (Graphite). | 3,013 | Uthamini umekamilika, watu 723 wamelipwa Tshs. 6.4 bilion, Watu 47 hawajachukua hundi zao. |
| TPDC/Kampuni ya Ferrostaal ya Ujerumani. | Wilaya ya Kilwa. Eneo la Kiwanja Na. 1. Kitalu K Kilwa Mjini. | Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea. | 60 | Usanifu mradi na uthamini wa mali katika eneo hilo umekamillika. |
| M/s. Oyo Real Estate Co. Ltd. | Wilaya ya Kilwa. Vijiji vya Mtandi na Rushungi | Viwanda vya mazao ya mafuta. | 1,426. | Mpango wa matumizi ya ardhi na uhawilishaji umekamilika. |
| STATOIL, EXONMOBIL, OPHIR ENERGY | Manispaa ya Lindi. Eneo la Kikwetu. | Ujenzi wa Mtambo wa Gesi Asilia. | 2,071 | Upimaji ardhi, utoaji Hatimiliki, Uthamini, Tathmini ya mazingira (E&S.I.A) imekamilika. |
| PACCO GEMS Ltd. | Wilaya - Ruangwa. Manispaa ya Lindi Eneo la Mtange. | Uchimbaji wa madini ya kinywe | 2,169.6 | Uthamini umefanyika. Fidia imelipwa kwa watu 52. |
| Bodi ya Korosho | | Viwanda vya magunia, salfa, na | 50 | Uthamini umekamilika na fidia ya Tshs. 108 millioni imelipwa. |

| Kampuni ya Uwekezaji | Mahali anapowekeza. | Matumizi ya ardhi | Ukubwa (ha.) | Hali halisi |
|---|---|---|---|---|
| Tanzania. | | ubanguaji korosho. | | |

## UTENGAJI WA MAENEO YA VIWANDA NA MAENEO YA WAJASIRIAMALI.

Katika mkoa wa Lindi halmashauri zote sita zimeanza kuweka mipango ya kutenga maeneo ya uwekezaji, maeneo ya viwanda na maeneo kwa ajili ya wajasiriamali wadogowadogo. Kwa mwaka 2016/2017 halmashauri ya manispaa ya Lindi imetenga eneo la ekari 150 kwa ajili ya ujenzi wa chuo kikuu, maeneo sita (6) kwa ajili ya wajasiriamali na imepanga kupima viwanja 2,000 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa imetenga ekari 100 kwa ajili ya viwanda na maeneo mawili (2) kwa ajili ya wajasiriamali. Wilaya ya Liwale imetenga ekari nne (4) kwa ajili ya wanawake na vijana. Wilaya ya Nachingwea ilitenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara mia tano na thelathini (530). Wilaya ya Kilwa imetenga ekari 6.37 na wilaya ya Lindi imetenga viwanja 350 kwa ajili ya wafanyabishara ndogondogo.

## MIGOGORO YA ARDHI.

Kwa mwaka 2016/2017 mkoa ulikuwa na lengo la kuanzisha kamati za kutatua migogoro ya ardhi na kuhakikisha kuwa zinafanya kazi hiyo kwa ueledi mkubwa. Kamati hizo zimeanzishwa katika ngazi ya mkoa, wilaya na halmashauri na kufanya kazi ya kushughulikia kero, malalamiko, madai, na fidia ya ardhi katika halmashauri za wilaya na halmashauri ya manispaa. Halmashauri zote sita za mkoa zimeanzisha kamati za kusikiliza na kusuluhisha malalamiko ya ardhi na madai ya fidia hii ikiwa ni asilimia 100 ya lengo lililokusudiwa. Hadi kufikia April, 2017 halmashauri ya manispaa na halmashauri za wilaya zilishughulikia migogoro 82.

## MIGOGORO YA MIPAKA YA WILAYA NA VIJIJI.

Katika usuluhishi wa migogoro ya mipaka ya wilaya na vijiji lengo la mkoa lilikuwa ni kusaidiana na mamlaka za serikali za mitaa kusuluhisha migogoro ya mipaka kati ya wilaya na wilaya, mipaka kati ya vijiji na vijiji na migogoro ya wakulima na wafugaji. Aidha, kazi nyingine ilikuwa ni kukusanya taarifa za maeneo yote yenye migogoro na kutambua chanzo cha migogoro hiyo.

Matokeo ya utekelezaji wa kazi hii yalikuwa kama ifuatavyo: -

i. Maeneo ya wakulima na wafugaji yalitengwa kwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika wilaya za Kilwa, Lindi na Nachingwea. Migogoro ya aina hiyo imebainishwa na kamati niliyoiunda na kwa sasa mimi na viongozi wenzangu wa mkoa tunashughulikia migogoro hiyo kwa pamoja.

ii. Mgogoro ya mpaka wa wilaya ya Kilwa katika (kijiji cha Nanjirinji A) na wilaya ya Liwale katika kijiji cha Mirui. Usuluhishi wa mgogoro huu unaendelea. Timu iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa inakamilisha kazi ya kupata Tangazo la Kisheria la Serikali (G.N.) kuhusu mpaka huo.

iii. Taarifa ya utambuzi wa maeneo yote yenye migogoro ya mipaka ya wilaya na wilaya na vijiji na vijiji ilikamilika katika mwaka 2016/2017 na migogoro hiyo inaendelea kufanyiwa kazi na viongozi wa Wilaya husika.

iv. Mkoa umeitisha kikao cha wadau 29/09/2017 kwa ajili ya kuweka mikakati ya kupunguza au kumaliza kabisa migogoro hiyo.

## CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA ARDHI NA MIPANGO MIJI.

Mkoa wa Lindi una changamoto mbalimbali zifuatazo katika maendeleo ya sekta ya ardhi;

i. Mkoa wa Lindi una upungufu wa wataalamu katika fani za upimaji ardhi, mipangomiji, ardhi, na uthamini mali na hasa katika halmashauri za Liwale, Nachingwea, Ruangwa na Lindi.

ii. Ukosefu wa vifaa vya kisasa vya upimaji na mipangomiji upungufu mkubwa wa vifaa vya upimaji (Total Station, GPS), vifaa vya kuchorea na vifaa vya ofisi (kompyuta, virudufu n.k.} hasa katika halmashauri za wilaya ya Lindi, Liwale na Ruangwa unarudisha nyuma kasi ya upimaji na upangaji miji.

iii. Ufahamu mdogo wa wananchi juu ya sera, kanuni na sheria za ardhi unakwamisha upangaji wa matumizi bora ya ardhi vijijini, maendeleo ya upimaji na upangaji wa miji, upimaji viwanja na mashamba.

iv. Mkoa wa Lindi kutokuwa na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

v. Wananchi wa wilaya za Kilwa, Nachingwea na Ruangwa kutopata huduma za Baraza la Ardhi, na Nyumba kutokana na umbali mrefu wa kupata huduma hizo mkoani wakati mabaraza yalishaanzishwa katika maeneo yao.

## SHIRIKA LA NYUMBA (NHC).

Shirika la Nyumba la Taifa kwa ujumla wake limejikita katika kusimamia na kuendeleza miliki kwa kujenga nyumba za gharama nafuu na zile za watu wa kipato cha kati na cha juu. Shirika la nyumba mkoa wa Lindi limefanikisha kukamilisha ujenzi wa nyumba 30 za makazi za gharama nafuu katika eneo la Mtanda ambazo nyingi zimenunuliwa na wakazi wa mkoa wa Lindi. Aidha, shirika limeweza kufundisha vijana wapatao 240 katika wilaya zote za mkoa jinsi ya kutumia mashine za kutengeneza matofali yakufungamana (interlocking blocks) na jinsi ya kujenga nyumba kwa kutumia matofali hayo.

Shirika limeendelea na jukumu lake la kawaida la kuboresha miundombinu ya nyumba ilizopangisha kwa kurekebisha miundombinu ya umeme, mifumo ya maji taka na maji safi na kupaka rangi ndani na nje ya nyumba hizo. Katika kutimiza azma ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu shirika lilitafuta na kupata viwanja 50 eneo la Mitwero, ardhi ya ekari 13 eneo la Tipuli na eneo la “National” kuna viwanja ambavyo bado havijaendelezwa.

## LENGO LA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2017/2018.

Kwa mwaka 2017/2018 Shirika la Nyumba lina mpango wa kujenga jengo la biashara (Biashara Complex) la ghorofa mbili eneo la (National) Mtanda. Shirika pia linatarajia kupata maeneo katika halmashauri ya wilaya ya Kilwa, Liwale na Nachingwea kwa mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kujenga nyumba za gharama nafuu.

## UKARABATI WA BANDARI YA LINDI

Kazi ya ukarabati wa Bandari ya Lindi ilianza tarehe 29 Mei, 2015 na ulitegemewa kukamilika ifikapo tarehe 5 Septemba, 2016 kwa gharama ya Sh. 3.11 bilioni. Mradi huu unatekelezwa na kampuni ya kizalendo ijulikanayo kwa jina la M/S COMFIX AND ENGINEERING LTD unahusisha ujenzi wa kalavati kwa ajili ya kupitisha maji, uondoaji wa mchanga kwenye eneo la gati, uwekaji maboya ya kuongozea meli na ujenzi wa "Mooring Dorphin" kwa ajili ya ufungaji wa kamba za meli. Hadi sasa mkandarasi amekamilisha ujenzi wa "Box Culverts" kumi (10) za zege zenye urefu wa mita 46 sawa na asilimia 48 ya kazi yote.

Kazi hii ilisimama kwa muda toka mwezi Septemba, 2016 kutokana na hitaji la maboresho muhimu yanayohusisha ujenzi wa kuta za zege ***(construction of Jetty head reinforcement concrete wall)*** ili kuimarisha sehemu ya maegesho ya meli (gati) na ujenzi wa ukuta wa zege kwa ajili ya kukinga maji ***(sea wall)*** na kazi hizi hazikuwa sehemu ya makubaliano ya awali.

Mamlaka ya bandari imeshakamilisha taratibu za zabuni ya kazi zilizojitokeza (addendum) ambazo hazikuwemo katika mpango wa kazi za awali. Aidha, kwa mujibu wa ratiba rejewa kati ya TPA na mkandarasi kazi ya ukarabati wa Gati katika Bandari ya Lindi inategemea kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2017.

## UWANJA WA NDEGE WA LINDI

Kiwanja cha ndege cha Lindi kina uwezo wa kupokea ndege mpaka yenye kiwango cha kuchukua abiria 80 (code 3c) hivyo Bombardier DH8 ina uwezo wa kutua. Kwa sasa maboresho yanahitajika katika jengo la abiria, barabara ya kuingia kiwanjani (access road) ambayo ni km 4 toka barabara kuu ya Lindi - Dar Es Salaam na baadhi ya maeneo ya kutua na kuruka ndege (run ways). Kiwanja kimetengewa kiasi kidogo cha bajeti kwa ajili ya ukarabati wa paa la jengo la abiria ambalo linavuja wakati wa mvua katika mwaka huu wa fedha. Katika mipango ya muda mrefu, kiwanja hiki ni miongoni mwa viwanja 11 vya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vinavyofanyiwa upembuzi yakinifu na mara baada ya kukamilika inatarajiwa kuwa pesa itatengwa katika bajeti ijayo ili kiweze kuboreshwa.

Kwa sasa kiwanja kina changamoto ya ukosefu wa gari la zimamoto ambapo tupatapo pindi ziara za ndege za viongozi au nyinginezo zinapokuja Lindi hulazimika kuazima gari toka kikosi cha zimamoto kabla ya ndege kutua na kuondoka kulingana na maelekezo ya sheria ya usalama wa anga na baada ya shughuli kuisha gari hilo huondoka.

## HALI YA UWEKEZAJI KATIKA MKOA

Tunavyo viwanda vidogo zaidi ya sitini (60) na tayari tumeshatenga maeneo kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kati na vikubwa ikiwemo mradi wa Liquefied Natural Gas (LNG), kiwanda cha mbolea, simenti, kubangua korosho, kutengeneza magunia, madini ya risasi, na viwanda vya mihogo. Tayari tuna kiwanda cha kubangua korosho na kutengeneza mafuta cha "SunShine Industrial Co Ltd" eneo la Mtama. Uwekezaji huu utachangia upatikanaji wa ajira, uongezaji kipato na upunguzaji umaskini.

## HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI

Serikali imeagiza mapato yote yakusanywe kupitia mfumo wa kielektroniki na kwamba mifumo hiyo ifungwe kwenye vyanzo vya mapato na kwa sasa mfumo huu umefungwa na unatumika katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikadiria kukusanya jumla ya Sh. 15,668,105,000/=.

Hadi kufikia Juni 30, 2017 Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekusanya jumla ya Sh. 14,139,375,836/= ambayo ni sawa na asilimia 90 ya lengo. Mkoa unaendelea kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kufanya vikao kati ya wataalamu na viongozi wa kuchaguliwa ili kujadili na kuweka mikakati bora ya ukusanyaji wa mapato ndani katika mkoa.

**MBIO ZA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2017**

Kwa mwaka 2016 mkoa wa Lindi ulishika nafasi ya kwanza kitaifa kwa kuwa na wastani wa alama 56.99 na halmashauri ya wilaya ya Lindi ilishika nafasi ya kwanza kitaifa, manispaa ya Lindi ilishika nafasi ya kwanza kikanda yenye mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Rukwa, Katavi na Kigoma. Matokeo haya kwa kiasi kikubwa yalitokana na jinsi mkoa wa Lindi ulivyojipanga kwa mwaka 2016.

Mwaka 2017 mkoa wa Lindi ulipokea Mwenge wa Uhuru kutoka mkoa wa Mtwara mnamo tarehe 21/5/2017 na kukimbizwa katika halmashauri zote sita na hatimae kuukabidhi mkoa wa Dar Es Salaam tarehe 27/5/2017 ukiwa salama. Katika mbio hizo jumla ya miradi 51 yenye thamani ya Tshs. 11,240,016,805/= ilipitiwa na Mwenge wa Uhuru. Ni matumaini yetu kuwa katika mbio za Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2017 mkoa wa Lindi tumefanya vizuri kama mwaka 2016.

**HITIMISHO**

Naomba taarifa hii ipokelewe rasmi na kuwa kumbukumbu za utekelezaji wa shughuli za serikali katika mkoa wa Lindi kwa kipindi cha 2016/2017 na Julai-Septemba, 2017.

Naomba kuwasilisha.

Ramadhani M. Kaswa

KATIBU TAWALA MKOA,

**LINDI.**

**28/09/2017**